

## **WATOTO 7,159 WAFANYA MTHANI WA KUHITIMU DARASA LA SABA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA 2020.**

Mnamo tarehe 7/10/2020 wanafunzi wa darasa la saba nchini kote wameanza mtihani wa kumaliza elimu yao ya msingi. Wilayani Kaliua, wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi jumla ni 7,159 wakiwemo wavulana ni 3,450 na wasichana 3,709. Watahiniwa hao wamegawanyika katika mikondo 318 ambayo ipo katika shule 101. Aidha, idadi hiyo ni 49.23% ya wanafunzi wote waliokusudiwa kufanya mtihani huo, na jumla ya wanafunzi 1,272 wameongezeka kwa mwaka huu, ikilinganishwa na wanafunzi 5,887 waliofanya mtihani huu mwaka 2019. Katika mtihani wa mwaka 2019, kiwango cha ufaulu kilikuwa ni 84%. Matarajio ya mwaka huu ni kufikia 90%.

Aidha, Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya ya Kaliua Ndg. Jerry D. Mwaga anawatakia wanafunzi wote wanaofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi heri na baraka katika mitihani yao. Pia anawaasa kuwa kumaliza elimu ya msingi siyo mwisho wa kujiendeleza kielimu.



Mkurugenzi wa halmashauri ya Kaliua Ndg. Jerry D. Mwaga akiwatakia heri wahitimu wa darasa la saba

Kwa upande wake afisa elimu msingi (W) Ndg. Martin Yohana Mahinda alisema maandalizi yalianza vizuri kuanzia usajili wa watahiniwa, semina kwa wasimamizi hadi kusambazwa kwa mithani, pia alisema kuwa watahiniwa wa mwaka 2020 wameongezeka kwa 2.03% ya watahiniwa wa mwaka jana.

Afisa Elimu Ndg. Martin Mahinda alisema pia matarajio yao baada ya mtihani kumalizika ni kuongeza ufaulu wa 5.37% kwahiyo kutoka 84.63 ya mwaka 2019

hadi 90% mwaka 2020. Mwisho alitoa ushauri kwa watahiniwa wanaomaliza darasa la saba kuwa, baada ya kumaliza waende shule za sekondari zilizopo karibu yao kwa ajili ya kuanza kujifunza masoma ya sekondari.



Afisa elimu msingi (W) Kaliua Ndg.Martin Mahinda akizungumza maandalizi ya mtihani wa taifa wa darasa la saba

Kwa upande wake mkuu wa shule ya msingi Ufukutwa Mwl Afrika Kitinya alisema, matarajio yake kwa watahiniwa kuwa wote watafanya vizuri na hatimaye kuendelea na kidato cha kwanza, pia aliwashauri watahiniwa baada ya kumaliza wafanye maandalizi ya kuingia pre form one, alisisitiza pia wawasaidie wazazi kazi na kuwa raia wema watakapokwenda.



Mwisho wanafunzi nao walisema Kuwa, Mtihani ni wakawaida hivyo wanatarajia kufanya vizuri katika mitihani yao.



Wanafunzi wanaohitimu darasa la saba wakipata chakula shule ya msingi ufukutwa baada ya kutoka kwenye mtihani.